JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

# TAARIFA KWA UMMA

## MWALIKO WA MAOMBI MAPYA NA UPANDISHAJI DARAJA WA LESENI ZA MAUDHUI YA REDIO ZA FM

1. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Na.12 ya mwaka 2003 yenye jukumu la kusimamia huduma za mawasiliano ya Kielektroni na Posta nchini Tanzania.

2. Kwa mujibu wa Kanuni za Taratibu za Utoaji Leseni, Tangazo la Serikali Na.422 la mwaka 2014, TCRA imeainisha Masafa kwa ajili ya utoaji wa Huduma za Maudhui ya redio za FM. Hivyo dirisha la maombi ya leseni ya utoaji wa huduma za maudhui ya redio limefunguliwa katika maeneo yafuatayo:-

| Mkoa | Eneo la Huduma | Idadi ya Masafa ya FM yaliyopo |
|---|---|---|
| Shinyanga | Shinyanga | **3** |
| Tanga | Tanga | **3** |
| Dodoma | Dodoma | **4** |
| Njombe | Njombe<br>Ludewa<br>Wanging'ombe<br>Makete<br>Makambako | **17** |
| Kigoma | Buhigwe<br>Kigoma<br>Kasulu<br>Kibondo<br>Uvinza<br>Kakonko | **6** |
| Mtwara | Newala<br>Nanyumbu<br>Tandahimba | **9** |
| Simiyu | Bariadi<br>Busega<br>Itilima<br>Maswa<br>Meatu | **28** |

| Mkoa | Eneo la Huduma | Idadi ya Masafa ya FM yaliyopo |
|---|---|---|
| Singida | Singida<br>Manyoni<br>Ikungi<br>Mkalama<br>Iramba | **13** |
| Rukwa | Sumbawanga<br>Sumbawanga Vijijini<br>Kalambo<br>Nkasi | **21** |
| Manyara | Hanang<br>Kiteto<br>Mbulu<br>Simanjiro<br>Babati | **10** |
| Ruvuma | Mbinga<br>Nyasa<br>Tunduru<br>Songea<br>Namtumbo | **10** |
| Lindi | Lindi<br>Nachingwea<br>Kilwa<br>Mtama<br>Liwale<br>Ruangwa | **20** |
| Mara | Musoma<br>Rorya<br>Serengeti<br>Tarime<br>Butiama<br>Bunda | **14** |
| Iringa | Iringa<br>Kilolo<br>Mafinga<br>Mufindi<br>Iringa Vijijini | **14** |

CREATING A LEVEL PLAYING FIELD

| Mkoa | Eneo la Huduma | Idadi ya Masafa ya FM yaliyopo |
| --- | --- | --- |
| Tabora | Tabora<br>Igunga<br>Kaliua<br>Urambo<br>Nzega<br>Uyui<br>Sikonge | **10** |
| Kagera | Karagwe<br>Misenyi<br>Muleba<br>Ngara<br>Biharamulo | **6** |
| Katavi | Mpanda<br>Nsimbo<br>Tanganyika<br>Mlele | **24** |

3. Waombaji wanatakiwa kuzingatia Mwongozo wa uwasilishaji wa maombi unaopatikana katika tovuti ya TCRA: **www.tcra.go.tz**.

4. Maombi yote ya utoaji wa huduma tajwa hapo juu yawasilishwe kupitia mfumo wa maombi ya leseni wa TCRA uitwao **Tanzanite Portal** kupitia kiunganishi kifuatacho: **https://tanzanite.tcra.go.tz/index.htm** kabla ama ifikapo tarehe 23 Juni 2025.

5. Tafadhali zingatia kwamba, endapo waombaji katika eneo fulani la huduma watajitokeza wengi zaidi ya kiasi cha Masafa yaliyoainishwa katika eneo hilo, TCRA itaweka Masafa ya eneo husika katika mchakato wa ushindani, yaani zabuni / Mnada.

6. Waombaji watakaoingia kwenye mchakato wa ushindani wa zabuni au mnada watajulishwa ili waweze kuwasilisha zabuni zao katika bahasha iliyofungwa ambayo itafunguliwa mbele ya wazabuni wote.

Imetolewa Tarehe **23 Aprili 2025.**

Digitally Signed By JABIRI KUWE BAKARI
Wed Apr 23 23:32:24 EAT 2025

Dkt. Jabiri K. Bakari
**MKURUGENZI MKUU**

Jengo la Mawasiliano, Na. 20 Barabara ya Sam Nujoma, S. L. P 474, 14414 DAR ES SALAAM, TANZANIA.
**Simu:** +255 22 2199760-9 / +255 22 2412011-2 / +255 784558270-1 **Nukushi:** +255 22 2412009-10
**Barua pepe:** barua@tcra.go.tz, dg@tcra.go.tz, **Tovuti:** www.tcra.go.tz

# MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA







**MWONGOZO WA UWASILISHAJI MAOMBI YA LESENI ZA MAUDHUI YA UTANGAZAJI (UTANGAZAJI WA BIASHARA – RADIO) KUPITIA MWALIKO WA MAOMBI (ITA)**

**Aprili, 2025**

## 1. UTANGULIZI

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ni Taasisi ya Serikali iliyoanzishwa chini ya Sheria ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania, Na.12 ya 2003 yenye jukumu la kusimamia sekta ya mawasiliano ya kielektroniki na posta katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania pamoja na huduma za utangazaji Tanzania Bara. TCRA inatoa mwongozo huu wa maombi ya leseni za maudhui ya utangazaji wa redio (Utangazaji wa Biashara) na uwasilishaji wa maombi hayo kwa njia ya mwaliko (Invitation to Apply – ITA).

Maombi yote ya leseni yanafanyika mtandaoni kupitia mfumo wa maombi ya leseni wa TCRA uitwao *Tanzanite Portal* kupitia kiunganishi kifuatacho: https://tanzanite.tcra.go.tz/login.htm.

## 2. SIFA ZA MWOMBAJI WA LESENI

a) Mwombaji anatakiwa awe ni Kampuni iliyosajiliwa na BRELA au Taasisi/Shirika/Asasi ambayo imesajiliwa na vyombo husika vya usajili.
b) Waombaji ambao tayari wana Leseni za Utangazaji wa redio wanatakiwa wawe wamekamilisha malipo yote ya ada za leseni na wahakikishe wana leseni hai kabla ya kufanya maombi mapya.

## 3. UTARATIBU WA MAOMBI YA LESENI BINAFSI

a) Mwombaji yeyote anayetaka kuomba leseni atafungua akaunti katika mfumo wa maombi ya leseni wa TCRA uitwao Tanzanite Portal kupitia kiunganishi: https://tanzanite.tcra.go.tz/login.htm
b) Mwombaji anahitajika kuandaa taarifa au nyaraka zifuatazo ili kupakiwa kwenye mfumo: -

**A. Kwa Ujumla**

i) Malipo ya Ada ya Maombi
- Ada ya Maombi ya Sh. 1,600,000 kwa Waombaji Wapya – Aina ya Leseni ya Wilaya;
- Ada ya Maombi ya Sh. 1,600,000 kwa Waombaji wanaopanda kutoka kuwa na leseni ya Kiwilaya hadi Kimkoa (upgrade);
- Ada ya Maombi ya Sh. 3,200,000 kwa Waombaji wanaopanda kutoka kuwa na leseni ya Kimkoa hadi Kitaifa (upgrade);

ii) Ada ya maombi italipwa kabla ya dirisha la uombaji wa leseni za maudhui ya utangazaji wa redio (Utangazaji wa Biashara) halijafungwa tarehe **16, Juni 2025**. Maombi yatakayolipwa baada ya tarehe hiyo hayatakubaliwa kazi.

iii) Nakala iliyoidhinishwa ya nyaraka za usajili kwa Kampuni (Memorandum and Articles of Association) au Katiba kwa Mashirika au Asasi zisizo za Kiserikali (Certified copy of Memorandum and Articles of Association or constitution for registered societies and NGOs);
Zingatia sharti la umiliki wa hisa kwa mujibu wa Kanuni ya 22 (1) (b) ya Kanuni za Leseni za Mwaka 2018 *inayomtaka Mwombaji Leseni ya Maudhui kuwasilisha nyaraka za Kampuni inayoonesha Kampuni inayoomba Leseni inamilikwa na Mtanzania kwa asilimia zisizopungua hamsini na moja*.

iv) Nakala iliyothibitishwa ya cheti cha Usajili wa Jina la kituo;
v) Nakala iliyothibitishwa ya cheti cha Usajili kwa kampuni zilizosajiliwa;
vi) Nakala iliyothibitishwa ya cheti cha Usajili kwa vyama au mashirika yaliyosajiliwa;
vii) Nakala iliyothibitishwa ya cheti cha Wadhamini Waliosajiliwa (Majina ya wadhamini yaambatishwe);
viii) Nakala iliyothibitishwa ya cheti cha Namba ya Utambulisho wa Mlipakodi (TIN);
ix) Nakala iliyothibitishwa ya hati safi ya kodi (Tax clearence Certificate) inayotumwa kwenda TCRA;
x) Uthibitisho wa uraia wa wanahisa (Pasipoti, Cheti cha Kuzaliwa, au Kitambulisho cha Taifa); na
xi) Tovuti na anwani za baruapepe (Zingatia: Usajili wa Majina ya Vikoa ni lazima uwe umetumia msimbo wa nchi (dot tz country code top level domain – ccTLD).

**B. Mpango wa Biashara**

Mpango Mahsusi wa biashara (Business Plan) unapaswa kujumuisha maudhui/nyaraka zifuatazo;

i) Wasifu wa Kampuni au Taasisi;
ii) Muhtasari wa malengo, maono na dhamira ya kuanzishwa kwa mradi wa utangazaji;
iii) Miongozo, vipeperushi na maelezo ya kiufundi ya vifaa vitakavyotumika;
iv) Ratiba ya utekelezaji wa mradi na mpango wa ujenzi;
v) Taarifa kuhusu rekodi / uzoefu (marejeleo);
vi) Maelezo kuhusu Huduma itakayotolewa;
vii) Muundo wa gharama na bei ya Huduma;
viii) Makadirio ya msingi kuhusu wigo wa wateja;
ix) Mkakati wa maendeleo ya rasilimali watu;
x) Mkakati wa huduma kwa wateja (kuhakikisha ubora wa huduma);
xi) Ujenzi wa kituo, mchoro wa mpangilio, vifaa na viwango vya utangazaji kama inavyoelekezwa na muhtasari katika **Kiambatisho I**;
xii) Sera ya uhariri ya kituo (Kanuni za Maadili ya Kituo) kulingana na kielelezo kilichoidhinishwa na TCRA (kilichoambatishwa kama **Kiambatisho II**) na maudhui yawe kama ilivyoainishwa katika Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroni na Posta (Maudhui ya Redio na Televisheni), za 2018;
xiii) Mpango wa kina wa vipindi vya Siku 7 unaotarajiwa ambao unaakisi muundo ulioidhinishwa na TCRA ulioambatishwa kama **Kiambatisho III** cha Muongozo huu kwa kuzingatia sifa zifuatazo. -
    a) Ubora na aina (variety);
    b) Manufaa kwa uchumi wa ndani;
    c) Kupanua uchaguzi wa programu, ikijumuisha programu za watoto kwa mujibu wa mahitaji yaliyotolewa chini ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroni na Posta (Maudhui ya Redio na Televisheni), ya 2018 kwa muda na kiasi (duration and quota); na

d) Athari kwa manufaa ya maendeleo ya sekta ya utangazaji kwa ujumla

xiv) Taratibu za udhibiti wa ubora wa maudhui ya utangazaji;

xv) Muundo wa Shirika au menejimenti; na

xvi) Wasifu binafsi (CV) kwa watendaji wakuu.

Pendekezo la biashara pamoja na viambatisho vyake vinavyohusika vitakuwa kwa kifupi na kwa muhtasari vikilenga leseni iliyoombewa, na mada zake zitakuwa kwa mujibu wa Muundo wa Kielezo cha pendekezo la mradi ulioambatishwa pamoja na mwongozo huu kama **Kiambatisho IV**.

## 4. ENEO LA HUDUMA LA LESENI

a) Eneo la huduma kwa ajili ya huduma ya maudhui ya Kimkoa (Utangazaji wa Redio) ni upeo wa pointi kumi (mikoa ya utangazaji) za upatikanaji.

b) Eneo la huduma kwa ajili ya leseni ya huduma za maudhui ya Wilaya ni upeo wa sehemu tatu za upatikanaji ndani ya eneo la utawala wa kimkoa.

## 5. TATHMINI YA MAOMBI

a) TCRA itafanya tathmini ya maombi yote kulingana na vigezo vilivyoainishwa katika mwongozo huu kwa kuangalia uwezo wa kiufundi, maudhui, uzoefu wa utoaji huduma za redio na mchanganuo wa kifedha; na ametimiza sifa za mwombaji kama iivyoelekezwa kwenye Sehemu ya 2 ya mwongozo huu. Vigezo vya tathmini kwa wenye sifa za uombaji wa leseni ni kama ilivyoainishwa kwenye **Kiambatisho V**.

b) Endapo waombaji waliofuzu katika eneo fulani la huduma ni wengi zaidi ya idadi masafa ya iliyopo: -

i.) ***TCRA itayaingiza masafa hayo katika mchakato wa ushindani yaani zabuni/ Mnada.***

ii.) Wale ambao wataingia kwenye ***mchakato wa ushindani wa zabuni au mnada watajulishwa kuwasilisha zabuni zao katika bahasha iliyofungwa vyema ambayo itafunguliwa mbele ya wazabuni wote***.

iii.) Maelezo ya uthamini kwa njia ya ushindani yanapatikana kama **Kiambatisho VI.**

**KIAMBATISHO I**

## A. MAHITAJI YA JUMLA YA KITUO CHA UTANGAZAJI

| S/N | KIPENGELE | VIGEZO VINAVYOTAKIWA |
|---|---|---|
| i. | TAA YA KUONESHA KUWA STUDIO IKO HEWANI | Ni lazima taa ya kuashiria kipindi kinaenda hewani ifungwe kwenye lango la chumba cha studio juu nje na ndani ili kuwataarifu watu kuhusu shughuli zinazofanyika ndani ya studio. |
| ii. | KELELE NA UDHIBITI WA SAUTI NDANI YA CHUMBA CHA STUDIO | Vyumba vya studio lazima vufungwe mfumo maalumu wa kuzuia sauti (kutoka au kuingia studio wakati kipindi kinaendelea) na mwangwi ili kuwezesha usikivu madhubuti usio na mwingiliano wa sauti au mwangwi kwa wasikilizaji. |
| iii. | UDHIBITI JOTO WA CHUMBA NA HEWA | Vyumba vya utangazaji vya studio sharti viwe na hewa ya kutosha na/au vidhibiti joto kwa ajili ya afya na usalama wa watumiaji na uendeshaji bora wa vifaa vya studio (mfano: viyoyozi, n.k.). |
| iv. | VIPIMO VYA CHUMBA CHA MATANGAZO (LIVE) | Chumba cha utangazaji sharti kiwe na eneo lisilopungua mita za mraba 16 ($m^2$16) na urefu wa angalau mita 2.5 kutoka sakafuni hadi darini ili kuwa na nafasi ya kutosha katika uendeshaji wake. |
| v. | VIPIMO VYA CHUMBA CHA UTENGENEZAJI WA VIPINDI | Chumba cha utengenezaji wa vipindi sharti kiwe na eneo lisilopungua mita za mraba 16 (16 $m^2$) na urefu wa angalau mita 2.5 kutoka sakafuni hadi darini ili kuwa na nafasi ya kutosha katika uendeshaji wake. |
| vi. | VIPIMO VYA CHUMBA CHA UANDAAJI NA UTAFUTAJI WA HABARI | Chumba cha uandaaji na utafutaji sharti kiwe na eneo lisilopungua mita za mraba 16 (16 $m^2$) na urefu wa angalau mita 2.5 kutoka sakafuni hadi darini ili kuwa na nafasi ya kutosha katika uendeshaji wake. |
| vii. | UMEME MBADALA (POWER BACKUP) | Mfumo wa mbadala wa nishati sharti ufungwe kwenye jengo la studio na mahali pa kurushia matangazo ili kuhakikisha kuwa kituo kinakuwa hewani hata wakati ambapo nishati ya umeme mkubwa inapokata. |
| viii. | HATUA ZA USALAMA DHIDI YA MOTO | Vifaa vya kuzima moto kama vile vizima moto sharti vifungwe kwenye jengo la studio na mahali pa kurushia matangazo |
| ix. | MUUNDO WA MNARA | Mnara sharti uwe na vitu vifuatavyo: -<br>a) Alama za rangi nyekundu na nyeupe;<br>b) Taa za tahadhari za ndege/ anga; na<br>c) Kinga dhidi ya umeme na radi. (Earthing and Electrical Protection) |
| x. | USALAMA | Ni sharti Studio iwe na uzio mzuri na udhibiti wa uingiaji wa kielektroni umefungwa kwenye chumba cha studio cha 'kurushia matangazo' na vyumba vingine vya studio. Mfano. bayometriki au Mifumo ya Smartcard, n.k. |

## B. MAHITAJI YA KIUNGO CHA TRANSMITA YA UTANGAZAJI

| NA. | KIPENGELE | VIGEZO VINAVYOTAKIWA |
|---|---|---|
| i. | ENEO LA UFUNGAJI | Transmita ya STL sharti ifungwe kwenye chumba cha kudhibiti/mitambo (control room) katika studio ya utangazaji, na kipokeaji cha STL kifungwe kwenye eneo la kurushia matangazo (transmitter site) |
| ii. | NJIA ZA KUUNGANISHA STUDIO NA MTAMBO WA KURUSHIA MATANGAZO | Njia za kuunganisha studio na mtambo wa kurushia matangazo ni sharti kutumia kiungo cha pointi kwa pointi (P2P) masafa ya (Microwave), mkongo wa mawasiliano, Kiungo cha IP, n.k. |

**C. MAHITAJI YA KIUFUNDI YA MFUMO WA UTANGAZAJI**

| NA. | KIPENGELE | VIGEZO VINAVYOTAKIWA |
|---|---|---|
| i. | CHUMBA CHA KURUSHA MATANGAZO (TRANSMITTER ROOM) | Chumba cha kurushia matangazo sharti kiwe na hewa ya kutosha ili kutunza vifaa vya utangazaji na kipokezi cha STL. |
| ii. | NGUVU YA USAMBAZAJI (TRANSMITTING POWER) | Ni sharti kurekebisha nguvu ya usambazaji wa matangazo ili kuepuka mwingiliano na vituo vingine vya redio na isizidi kipimo cha ERP kwa kiasi cha 10KW. |
| iii. | WIGO WA MASAFA | Transmita ya matangazo ya FM sharti ifanye kazi ndani ya bendi ya masafa ya 87.5 MHz hadi 108 MHz. Ni sharti transmita irekebike ili kukubali masafa yoyote yaliyokabidhiwa kwenye masafa yatakavotolewa na TCRA. |
| iv. | ENEO LA URUSHAJI MATANGAZO | Eneo la matangazo sharti liidhinishwe na TCRA. Jina la eneo na jira nukta (geographical coordinates) lazima vifafanuliwe vyema. |

**D. MAHITAJI YA KITUO CHA REDIO FM/ VIFAA VYA STUDIO**

| NA. | KIPENGELE | VIGEZO VINAVYOTAKIWA |
|---|---|---|
| i. | VIFAA VYA VYUMBA VYA MATANGAZO VYA STUDIO | Chumba cha studio sharti kiwe na vifaa vitakavyotumika katika huduma za Utangazaji. Vifaa hivyo ni pamoja na: -<br>a) Kichanganyaji Kitaalamu (Kichanganyaji kilichoteuliwa kwa ajili ya utangazaji wa redio) - *Professional Mixer/Audio Console/ radio panel/ sound panel, or sound desk (Mixer designated for radio broadcasting;*<br>b) Vipaza sauti (kimoja kwa kila Mtangazaji au mwenyeji na chache kwa ajili ya mgeni ikilazimu) - *Microphones (One for each Presenter or host and few for a guest if required)*;<br>c) Mvumo wa kipaza sauti au mkono au stendi - *Microphone boom or arm or stands*;<br>d) Vipokea sauti vya masikioni (Moja kwa kila Mtangazaji au mwenyeji na vingine kwa ajili ya mgeni ikilazimu - *Headphones (One for each Presenter or host and few for a guest if required);*<br>*e)* Kitafuta sauti cha FM (Kipokezi Kimezimwa) - *FM tuner (Off Air Receiver) ;*<br>*f)* Kiwambo cha spika - *Monitor speaker;*<br>g) Taa ya hewani iliyounganishwa na kudhibitiwa na Meza ya mixer - *On-air light Connected to and controlled by the Mixer Console*;<br>h) Kompyuta iliyofungiwa programu ya Playout na Automation;<br>i) Mseto wa simu - *Telephone hybrid*;<br>*j)* Mfumo wa simu wa kuruhusu kuongea tena (Si lazima) - *Phone Talkback system (Silazima);*<br>k) Intercom (Si lazima);<br>l) Spika za *Cue/preview* (Si lazima); na<br>m) Mita za Kiwango (Si lazima)- *Level Meter.* |
| ii. | CHUMBA CHA STUDIO CHA UANDAAJI WA MATANGAZO YA REDIO – (*RADIO PRODUCTION STUDIO ROOM)* | Chumba cha studio kinaweza kutumika kama chumba cha akiba hewani na lazima kiwe na vifaa vinavyoweza kutumika katika huduma za Utangazaji. Mahitaji yake ni kama ya chumba cha utangazaji. |

| | | |
|---|---|---|
| iii. | VIFAA VYA CHUMBA CHA UDHIBITI/MITAMBO (*CONTROL ROOM EQUIPMENT)* | Chumba cha kudhibiti/mitambo lazima kiwe na vifaa vitakavyotumika katika kuchakata Mawimbi ya FM kabla ya kusambazwa. Vifaa hivyo ni pamoja na:-<br>a) Seva ya Maudhui ya Matangazo - *Broadcast Content Server;*<br>b) Kiungo cha Studio kwenda kwenye Mtambo wa urushaji matangazo - *Studio to Transmitter Link (STL);*<br>c) Kichanganuzi cha FM - *Modulation monitor/FM analyser*; na<br>d) Jenereta ya FM stereo. |
| iv. | CHUMBA CHA HABARI/CHUMBA CHA KUHARIRI NA MAKTABA | Chumba cha Habari lazima kiwe na vifaa vinavyotumika katika kuhariri na kuhifadhi habari kama vile komputa zilizo na programu tumizi zinazowezesha kuandika habari na kuzihariri, Televisheni, kipokezi cha redio, meza na viti kwa ajili ya wanahabari. |

**E. MAHITAJI YA RASILI MALI WATU KWA AJILI YA KUENDESHA KITUO**

| NA. | KIPENGELE | VIGEZO VINAVYOTAKIWA |
|---|---|---|
| i. | Idadi ya wafanyakazi na elimu yao | Kiwango cha chini cha wafanyikazi<br>Meneja wa kituo - 1;<br>Watozi/Wazalishaji - 4;<br>Wawasilishaji - 4;<br>Mhariri mkuu - 1;<br>Mwandishi wa habari – 2; na<br>Mafundi - 2. |
| ii. | Elimu ya wafanyakazi | Diploma ya Uandishi wa Habari kwa Mhariri Mkuu, Watozi, Waandishi na Wawasilishaji wa habari. |

**Kiambatisho II**

**MWONGOZO WA SERA YA UHARIRI**

1. Jina la Kituo……………………………………………………………………

2. Umiliki: Binafsi ☐ Umma ☐

3. Soko: Jumuia ☐ Wilaya ☐ Kimkoa ☐ Kitaifa ☐

4. Aina ya Leseni: Umma ☐ Biashara ☐ Jumuia ☐

5. Maudhui yanayotolewa: -

| | |
|---|---|
| Dini | |
| Elimu | |
| Umma | |
| Biashara | |
| Siyo ya Kibishara | |
| Michezo | |
| Muziki | |
| Nyingine | |

6. Maelezo ya Jumla ya Shabaha ya Sera ya Uhariri ……….................……………
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………

7. Malengo mahususi ya Maudhui Yanayotolewa
……………………………………………………………………………………..
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………
………………………………………………………………………………………

8. Hadhira inayolengwa
………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
………………………………

9. Matokeo/Mafanikio Yanayotarajiwa
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………
…………………………………………………………………………………………………

10. Mwongozo

| NA. | MWONGOZO | MAELEZO YA MWONGOZO |
|---|---|---|
| 1 | Uadilifu | |
| 2 | Usawa | |
| 3 | Sifa Merit | |
| 4 | Uhuru wa Habari | |
| 5 | Taswira | |
| 6 | Faragha | |
| 7 | Uhuru wa Uhariri | |
| 8 | Kuaminika | |
| 9 | Kutopendelea | |
| 10 | Usahihi | |
| 11 | Mahojiano | |
| 12 | Msambao wa Uchguzi | |
| 13 | Matangazo Mbashara | |
| 14 | Simu zinazoingia | |
| 15 | Uandishi wa Habari za wananchi | |
| 16 | Mitandao ya kijamii kama chanzo cha habari | |
| 17 | Intaneti kama chanzo cha habari | |
| 18 | Vipindi vya Dini | |

| | | |
|---|---|---|
| 19 | Ladha na adabu – *taste and decency* | |
| 20 | Vipindi vya Afya | |
| 21 | VVU na UKIMWI | |
| 22 | Jinsia | |
| 23 | Watoto | |
| 24 | Maudhui kwa hadhira ya watu wazima - *Watershed* | |
| 25 | Uhalifu na Kupinga Shughuli za Kijamii - *Crime and anti Social Activity* | |
| 26 | Mtangazo kuhusu maafa | |
| 27 | Ukatili | |
| 28 | Ripoti kuhusu Vita | |
| 29 | Machafuko, Utekaji nyara na Mateka | |
| 30 | Maonyo ya mabomu | |
| 31 | Maandamano | |
| 32 | Taratibu za Kushughulikia Malalamiko | |
| 33 | Huduma kwa wateja | |

**Msimamo mwingine wowote wa sera za kituo.**

Mimi..............................................., Ofisa Mtendaji Mkuu wa kituo, ninatamka kwamba taarifa iliyotolewa hapo juu, kulingana na uelewa wangu, ni ya kweli na sahihi.

Ikiwa imetolewa vinginevyo inaweza kuondoa sifa za kituo changu kufikiriwa kupewa Leseni.

**JINA LA OFISA MTENDAJI MKUU WA KITUO:**

**SAINI:**

**TAREHE NA MHURI WA OFISI:**

**Kiambatisho III**

**PROGRAMU INAYOTARAJIWA YA KINA YA SIKU 7**

**[Ingiza siku]**

| Muda | Jina la Kipindi | Lengo mahususi | Hadhira inayolengwa | Mafanikio Yanayotarajiwa |
|---|---|---|---|---|
| 11:00-11:30 | Mfano: Mama na Watoto | Kuielimisha jamii kuhusiana na njia bora ya kuwalea Watoto | Wazazi | Malezi bora |
| 11:30-12:00 | Mfano: Muziki | Kuburudisha | Wote (Vijana na Wazee) | Kuielimisha jamii kuhusu masuala kadhaa kama vile UKIMWI, uhusiano kazini, kwa kutumia nyimbo. |

**[Ingiza siku]**

| Muda | Jina la Kipindi | Lengo mahususi | Hadhira inayolengwa | Mafanikio Yanayotarajiwa |
|---|---|---|---|---|
| | | | | |
| | | | | |
| | | | | |

**Kiambatisho IV**

## MUUNDO WA MAPENDEKEZO YA MRADI KWA AJILI YA MAOMBI YA LESENI

### 1.0 UTANGULIZI:

Maombi ya kituo cha Redio au Televisheni yanapaswa kuambatishwa na muhtasari wa vipengele muhimu (upembuzi yakinifu) ambapo mwombaji (waombaji) ataweza kutoa maelezo ya kina. Vipengele hivi vinaweza kujumuisha: Muhtasari wa kiutendaji, uchambuzi wa soko, masuala ya kiufundi, mfumo wa uongozi, uchambuzi wa kifedha na uwezekano wa mradi.

1.1 **Dira:** Ni kitu gani unachotaka kukifikia kwa kuanzisha Kituo kama hicho cha Redio au Televisheni?

1.2 **Dhamira:** Utafanya nini ili kufikia dira yako?

1.3 **Malengo:** Ni sababu gani zilizoleta msukumo wa kuanzishwa kwa kituo hicho.

1.4 **Eneo:** (mahali halisi) wapi unapanga kuanzisha kituo chako

1.5 Majina na anwani za waombaji na wanahisa zionyeshwe kwenye maelezo ya wasifu (CV) zitakazowasilishwa TCRA.

### 2.0 MCHANGANUO WA SOKO:

2.1 **Hali ya sasa:**

Ni sharti kuwe na maelezo ya hali ya sasa ya utangazaji ya eneo linalohusika unalotaka kuanzisha kituo chako.

2.2 **Kupenya kwa Biashara:**

Je, utawezaje kupenya au kuifikia hadhira unayoihitaji?

2.3 **Makadirio ya Biashara:**

Eleza uendelevu wa biashara yako ndani ya mwaka mmoja au miwili ijayo. Je, utaweza kuendeleza kituo? Jinsi gani?

### 3.0 UCHANGANUZI WA KIUFUNDI:

3.1 Studio na aina/maelezo, mpangilio na eneo ya vifaa vya transmita, Bainisha eneo la transmita za studio.

3.2 Aina za Antena

3.3 Ufungaji na kazi za ujenzi na vifaa (TX/studio)

3.4 Michoro na viambatisho sharti viambatishwe

3.5 Kiungo cha transmita na Studio (STL), mnara wa antena na eneo la litakalofikiwa na mawimbi ya utangazaji *(Coverage area)*

3.6 Kuzingatia uwepo na ubora wa umeme:

- Ugavi wa umeme utakaotumika (Umeme wa TANESCO, Jua, Jenereta n.k)
- Uwezo wa jenereta / UPS na aina zake
- Kidhibiti Umeme (Automatic Voltage Regulator) na uwezo wa vidhibiti umeme (stabiliser capacity)

## 4.0 MASUALA YA MAUDHUI:

4.1 Ratiba ya Vipindi

4.2 Vyanzo vya vipindi

## 5.0 MUUNDO WA MENEJIMENTI:

5.1 Muundo/ chati ya shirika

a) Wasifu wa Kampuni / Taasisi

b) Onesha nafasi ya uongozi, sifa na kazi zao,idadi ya wafanyakazi katika kila sehemupamoja na viwango vyao vya elimu na utaalam wao.

c) Onesha ajira ya wafanyakazi na toa maelezo ya wasifu (CV) za watendaji wakuu.

d) Onesha viwango vya juu vya elimu vya wafanyakazi wako muhimu, hii ni kwa meneja wa kituo, msimamizi wa vipindi wahariri, waandishi wa habari na mafundi.

5.2 Maendeleo/Mafunzo ya Wafanyakazi

a) Utatoaje mafunzo kwa wafanyakazi wako?

b) Utajumuishaje teknolojia mpya katika biashara yako?

## 6.0 MCHANGANUO WA KIFEDHA:

6.1 Mpango wa ufadhili (kuthibitisha uwezo wa kifedha wa mwombaji): -

a) Taarifa ya miezi sita (6) ya benki ya kampuni kwa kampuni zinazofanya kazi au za wanahisa kwa kampuni mpya; au

b) Barua ya ufadhili wa mradi kutoka kwa mfadhili au kutoka Benki inayotoa dhamana ya mkopo au msaada wa kifedha.

6.2 Taarifa za mapato yanayotarajiwa ya miaka mitano: Taarifa ya mapato, mtiririko wa fedha na mizania. Mpango inapaswa kushabihiana na jedwali lifuatalo: -

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | **HALI YA KIFEDHA** | | | | | |
| 1.1 | **MTAJI WA BIASHARA** | | | | | |
| 1.2 | Taarifa za Fedha tarajiwa | | | | | |
| | Mpango wa Ufadhili (Ufadhili wa Mradi) Upatikanaji wa Fedha | | | | | |
| | | **Mwaka1** | **Mwaka2** | **Mwaka3** | **Mwaka4** | **mwaka 5** |
| | Kiwango cha faida halisi | | | | | |
| | Mapato ya Usawa (Return on Equity) | | | | | |
| | Uwiano wa Sasa wa uwezo wa kampuni kulipa madeni ya muda mfupi (Current Ratio) | | | | | |
| | Uwiano wa Mapato ya Uwekezaji (Return on Investment) | | | | | |
| | Mwenendo wa ukuaji wa mapato kwa miaka 5 | | | | | |

6.3 Uwiano wa uwekezaji wa mitaji (Usawa: Deni – Equity:Debt);

6.4 Muundo wa gharama na bei ya Huduma;

## 7.0 HUDUMA KWA WATEJA

7.1 Makadirio ya msingi kuhusu wigo wa wateja;

7.2 Mkakati wa huduma kwa wateja (kuhakikisha ubora wa huduma);

## 8.0 HITIMISHO:

Katika hitimisho, sharti uweze kueleza **UTOSHELEVU WA MRADI** yaani manufaa kwa jamii, matarajio ya mapato, fursa za mafunzo ya ajira na jinsi malengo ya kampuni/taasisi yako yatakavyotimizwa.

Kiambatisho V

## VIGEZO VYA TATHMINI YA MAOMBI

**A. Kwa Waombaji Wapya wa huduma za Maudhui ya Redio**

| Na. | Kigezo | Alama [%] |
|---|---|---|
| 1. | Uwezo wa kiufundi | 20 |
| 2. | Maudhui (Uanuai (content diversity) na Uzingatiwaji wa Kanuni) | 40 |
| 3. | Idadi na sifa za wafanyakazi muhimu | 15 |
| 4. | Uwezo wa kifedha | 25 |
| **Total** | | **100** |

**B. Kwa Waombaji wa Upandishaji Daraja au kuongeza Maeneo ya huduma za Maudhui ya Redio**

| Na. | Kigezo | Alama [%] |
|---|---|---|
| 1. | Uwezo wa kiufundi | 10 |
| 2. | Uzingatiwaji wa Maudhui (Uanuai wa Maudhui na Uzingatiaji wa ratiba) | 30 |
| 3. | Idadi na sifa za wafanyakazi muhimu | 15 |
| 4. | Uwezo wa kifedha | 25 |
| 5. | Uzingatiwaji wa Kanuni na Miongozo | 20 |
| **Total** | | **100** |

**Alama ya chini kwa mwombaji aliyefaulu ni 70%**

**Kiambatisho VI**

## UTOAJI WA MASAFA KWA MCHAKATO WA USHINDANI

Endapo waombaji waliofuzu katika eneo fulani la huduma ni zaidi ya idadi iliyopo ya masafa, basi ***TCRA itapanga masafa ya redio chini ya mchakato wa kiushindani yaani zabuni/ Mnada.***

Wale ambao wataingia kwenye ***mchakato wa ushindani wa zabuni au mnada watajulishwa kuwasilisha zabuni zao katika bahasha iliyofungwa vyema ambayo itawasilishwa na kufunguliwa mbele ya wazabuni wote***.

### (a) Utaratibu wa maombi

Mwombaji chini ya mchakato wa ushindani atawasilisha vitu vifuatavyo wakati wa awamu ya maombi;

i. Fomu ya Maombi Iliyojazwa na Kusainiwa (**Kiambatisho A**)
ii. Ushahidi unaofaa kwamba watu wawili wanaotia saini kwenye Fomu ya Maombi wameidhinishwa ipasavyo na Mwombaji. Ushahidi stahiki utajumuisha:
    a. Azimio la Bodi kutoka kwa Mwombaji; na
    b. Hati isiyoweza kubadilika ya wakili *(irrevocable power of attorney).*
iii. Tamko lililojazwa na lililotiwa saini la kufuata sheria za Mchakato wa Tuzo (**Kiambatisho B**)

### (b) Uwasilishaji wa Zabuni

i. Wazabuni watakabidhi zabuni zao kupitia Fomu ya Zabuni Isiyobalika iliyotolewa katika **Kiambatisho C**.
ii. Wazabuni wataonesha bei ya zabuni (katika sehemu mbili za desimali) kwa kila Eneo la Huduma wanalotaka kupata katika Fomu ya Zabuni Isiyobadilika.
iii. Waombaji hawawezi kuwa na Masafa ya FM zaidi kwa kila eneo la huduma.
iv. Wazabuni watawasilisha Fomu ya Zabuni Iliyotiwa Muhuri isiyoweza kubadilika, iliyotiwa saini na kupigwa mhuri kwa kila kipindi cha mnada katika Tarehe ya Mnada.

### (c) Awamu ya Ufunguzi wa Zabuni

i. Wazabuni wote watahitajika kuwakilishwa ana kwa ana kulingana na hati waliyoiwasilisha TCRA kuwa wameruhusiwa kushiriki mnada
ii. TCRA itapokea na kuzingua zabuni zote mbele ya Wazabuni wote.
iii. TCRA itazipanga bei za zabuni kwa utaratibu wa kushuka (yaani, kuanzia bei ya juu hadi ya chini kabisa).
iv. Katika hali ambapo kuna kulingana kwa thamani ya zabuni, TCRA itazipanga bei za zabuni kwa kufuata mpangilio wa alfabeti (kutoka A hadi Z) ya majina ya Wazabuni ili kuondoa ufanano.
v. TCRA itaanza kugawa Masafa kwa Mzabuni wa juu zaidi na kisha kwa Mzabuni anayefuata kwa kuzingatia upatikanaji wa Masafa.

### (d) Hatua ya Leseni

i. Washindi wa zabuni watalipa Bei ya zabuni ya Masafa kwa ukamilifu.
ii. TCRA itaendelea na mchakato wa Utoaji Leseni kwa Washindi wa Mnada baada ya uhakiki wa malipo.

**Kiambatisho A**

## Fomu ya Maombi

| | |
|---|---|
| **Jina la Mwombaji** | |
| **Anwani kamili** | |
| **Mawasiliano** | Jina ____________<br>Anwani ____________<br>____________<br>Baruapepe ____________<br>Simu ____________ |
| **Majina na vyeo vya watu 2 wanaotia saini kwenye Fomu ya Maombi** | <u>Mtu 1</u><br>Jina ____________<br>Cheo ____________<br><u>Mtu 2</u><br>Jina ____________<br>Cheo ____________ |
| **Watu (2) walioidhinishwa ambao watawajibika kutoa zabuni** | <u>Mtu 1</u><br>Jina ____________<br>Na. ya Kitambulisho (Na. ya Kitambulisho cha Taifa au Pasipoti)<br>____________<br>Anwani ____________<br>Baruapepe ____________<br>Simu ____________<br><u>Mtu 2</u><br>Jina ____________<br>Na. ya Kitambulisho (Na. ya Kitambulisho cha Taifa au Pasipoti)<br>____________ |

| | |
|---|---|
| | Anwani ____________________<br>Baruapepe ____________________<br>Simu ____________________ |
| **Saini zilizoidhinishwa** | Mtu 1<br>Saini ____________________<br>Tarehe ____________________<br>Mtu 2<br>Saini ____________________<br>Tarehe ____________________ |

Mhuri wa Kampuni/Taasisi: ____________________

Tarehe: __________________

**Kiambatisho B**

**Tamko**

(Mtu wa 1 Aliyeidhinishwa) ____________________, (Mtu wa 2 Aliyeidhinishwa) ________________________, na (Mtu wa 3 Aliyeidhinishwa) _______________________ wakiwa Mawakala Walioidhinishwa wa _______________ ("Mwombaji") (tu)natamka kwa niaba ya Mwombaji kwamba:

a. Mwombaji ana haki ya kushiriki katika Mchakato wa Tuzo na amepata vibali vyote muhimu vya kufanya hivyo;
b. Taarifa zilizomo na Maombi ya Mwombaji ni sahihi;
c. Kwa kadiri inavyowezekana kwa Mwombaji kufanya hivyo, Mwombaji anathibitisha kwamba haihusiani na au haijahusishwa na Mwombaji mwingine au chombo kingine ambacho kinaweza kutarajiwa kuwa Mwombaji mwingine;
d. Mwombaji atachukua hatua zote zinazostahili ili kuhakikisha kuwa Taarifa za Siri hazitolewi kwa mhusika mwingine isipokuwa wale wanaohitaji kupata Taarifa za Siri ili kutekeleza jukumu lao kuhusiana na ushiriki wa Mwombaji katika Mchakato wa Tuzo;
e. Mwombaji atajiepusha na kitendo chochote ambacho kinaweza kuwa na athari kwenye Mchakato wa Tuzo;
f. Mwombaji atazingatia Kanuni za Mchakato wa Tuzo kama zilivyo katika Makubaliano ya Habari;
g. Mwombaji anathibitisha kuwa ana rasilimali za kifedha ili kukidhi majukumu yake chini ya masharti ya Mkataba na kukidhi Vigezo na Masharti ya Leseni ikiwa ingepewa masafa kupitia Mchakato wa Tuzo.

Jina la Mwombaji: ___________________________________

**Imesainiwa kwa niaba ya Mwombaji**

Mtu wa 1 Aliyeidhinishwa: _________________________

Mtu wa 2 Aliyeidhinishwa: _________________________

Mtu wa 3 Aliyeidhinishwa: _________________________

(Saini ya watu hao ambao wamewezeshwa kumfunga Mwombaji au kuidhinishwa vinginevyo kumfunga Mwombaji).

Tarehe: _______________________ Mhuri wa Kampuni/Taasisi: ________________

**Kiambatisho C**

**Fomu ya Zabuni (Sealed Bid Form)**

Jina la Mwombaji:

______________________________________________

Eneo la Huduma: _____________

**TAMKO LA MASAFA AMBAYO MWOMBAJI ANAKUSUDIA YA KUTOA ZABUNI KATIKA MNADA WA MASAFA YA FM REDIO**

1. Onesha katika jedwali bei yako ya zabuni (katika sehemu mbili za desimali) kwa kila bendi ya FM.

| | Bei yako ya zabuni katika sehemu mbili za desimali (TZS) kwa kila bendi |
|---|---|
| Kwa tarakimu | |
| Kwa maneno | |

Ninatamka na kuahidi bila kubatilishwa kuwa Kampuni ya Mwombaji itagharimia Masafa Ilioainishwa kwenye Jedwali hapo juu kwa Bei ya Zabuni, iwapo atapewa masafa hayo.

Pamoja na tamko na ahadi iliyopo hapo juu, ninatamka na kuahidi bila kubadilika kuwa Kampuni ya Mwombaji italipia Masafa wa Vitalu kulingana na chaguzi za malipo mwishoni mwa Mnada, pale anapotangazwa kuwa Mshindi tarajali.

Ninatamka kwa dhati kwamba idadi ya Vitalu vya masafa iliyotajwa katika Maombi haya inaibana Kampuni ya Mwombaji kulipia kiasi hiki cha masafa kwa Bei ya Zabuni kwa kila Masafa wa Kitalu uliotajwa kwenye jedwali lililopo hapo juu iwapo itapewa katika Mnada huu wa Masafa

Tarehe: _________________

Jina la Mwakilishi Aliyeidhinishwa: ____________________________

Saini ya Mwakilishi Aliyeidhinishwa: _________________________

Mhuri wa Kampuni/Taasisi: __________________________



Wasiliana Nasi

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania
Mawasiliano Towers, 20 Barabara ya Sam Nujoma,
S. L. P. 474, Dar Es Salaam
+255 22 2199760 - 9 / +255 22 2412011 - 2 / +255 784558270 - 1
dg@tcra.go.tz | barua@tcra.go.tz